TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
TANZANIA
COMMISSION FOR HUMAN RIGHTS AND GOOD GOVERNANCE

LHRC
LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

# MUHTASARI WA RIPOTI KUHUSU HAKI ZA BINADAMU NA WAVUVI WADOGO KATIKA UPATIKANAJI NA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA BAHARI TANZANIA



## MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI WA AWALI

Aprili, 2026

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) ni taasisi huru ya serikali iliyoundwa kutetea, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na kuimarisha utawala bora nchini Tanzania. Inafanya kazi kama Taasisi ya Kitaifa ya Haki za Binadamu na pia Ofisi ya Mshauri Mkuu (Ombudsman), ambayo ni chombo cha kusikiliza na kushughulikia malalamiko ya wananchi.

Majukumu yake ni:- Kupokea na kuchunguza malalamiko kuhusu uvunjwaji wa haki za binadamu, na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora; Kufanya utafiti na kutoa elimu kwa umma ili kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu haki zao; Kukagua magereza, vituo vya polisi na maeneo mengine wanamozuiliwa watu, ili kuhakikisha haki za binadamu zinaheshimiwa; Kutoa ushauri kwa taasisi za umma na binafsi juu ya masuala ya haki za binadamu na utawala bora; Kufanya mapitio ya sheria na kupendekeza mabadiliko ya sheria ili ziendane na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu; Kufuatilia utekelezaji wa viwango vya kimataifa vya haki za binadamu; Kushirikiana na wadau wa kitaifa na kimataifa katika kulinda na kutetea haki za binadamu; na Kusuluhisha migogoro kwa njia ya mazungumzo na upatanisho. Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti yao: https://chragg.go.tz

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ni shirika la kufanya uchechemuzi kuhusu haki za binadamu nchini Tanzania. Kiliundwa mwaka 1995 kama shirika lisilo la kiserikali, lisilo la kibiashara, lisiloegemea upande wowote wa kisiasa, na linalojitolea kwa hiari.

Lengo kuu la LHRC ni kuwawezesha wananchi na kuwafundisha kuhusu sheria na haki za binadamu. Kupitia kazi zake, LHRC husaidia watu kuelewa haki zao, wajibu wao, na namna ya kuzilinda ili jamii iwe na usawa na haki. Kwa maelezo zaidi unaweza kutembelea tovuti yao rasmi: humanrights.or.tz.

Hii ni Taasisi ya Kitaifa ya Haki za Binadamu nchini Denmark. Iliundwa kwa jukumu la kukuza na kulinda haki za binadamu ndani ya Denmark na pia kimataifa. Kwa maelezo zaidi unaweza kutembelea tovuti yao rasmi: humanrights.dk.

Ripoti hii imeandaliwa na kuchapishwa kwa msaada wa kifedha kutoka Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Kimataifa la Sweden (Sida).

# JINA LA RIPOTI NA MCHAPISHAJI

**Jina la Ripoti:** Haki za Binadamu na Wavuvi Wadogo Katika Upatikanaji na Usimamizi wa Rasilimali za Bahari Tanzania.

**Mchapishaji:** Imechapishwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Aprili, 2026**.**

# SHUKRANI

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC wanatoa shukrani za dhati kwa wadau wote waliohusika kutoa taarifa na na takwimu zilizofanikisha uandaaji wa ripoti hii. Wadau hao ni pamoja na: Wizara ya Mifugo na Uvuvi (WMU); Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA) katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Tanga; Taasisi ya Utafiti ya Masuala ya Uvuvi Tanzania (TAFIRI); Timu ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Mwongozo wa Hiari wa Uvuvi Mdogo (NTT – SSF Guidelines);Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU); Jukwaa la Kitaifa la Wanawake wanaojishughulisha na Uvuvi Tanzania (TAWFA); wavuvi; wachakataji; na wauzaji wa mazao ya uvuvi.

Aidha, THBUB na LHRC wanatoa shukrani za dhati kwa timu ya wataalamu walioshiriki katika kukusanya taarifa na takwimu na uandaaji wa ripoti hii, akiwemo Bi. Bigeyo Kuboja ambaye ni mtaalamu wa uvuvi kutoka TAFIRI, kwa ushauri wake wa kitaalamu wakati wa mapitio ya nyaraka, na maandalizi ya ukusanyaji wa taarifa kwa wadau.

Vilevile THBUB na LHRC wanashukuru taasisi za serikali WMU, Wizara ya Katiba na Sheria na Mamlaka za Serikali za Mitaa, wavuvi wadogo, Vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali ya Uvuvi (BMUs), Mabaraza ya uhusiano wa Vijiji na Hifadhi za Bahari (VLCs) Maeneo Shirikishi ya Usimamizi wa Raslimali ya Uvuvi (CFMAs), TAWFA, Asasi za Kiraia, mashirika yasiyo ya kiserikali (Wildlife Conservation Society (WWF); Sea Sence; MWAMBAO network), na wadau wa maendeleo wakiwemo Shirika la Kimataifa la Chakula na Kilimo Duniani (FAO). Wadau hawa, walioshiriki na kutoa maoni yao ya kitaalamu katika warsha ya kitaifa ya wadau wa uvuvi iliyoandaliwa na THBUB Julai, 2025. Maoni yao yalisaidia kuboresha na kuthibitisha matokeo ya ripoti hii.

Kipekee, THBUB na LHRC wanaishukuru Taasisi ya Kitaifa ya Haki za Binadamu nchini Denmark (DIHR), kwa kufadhili kazi hii na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uzingatiaji wa haki za binadamu kwa wavuvi wadogo, katika usimamizi na upatikanaji wa rasilimali za bahari.

# 1. UTANGULIZI

Ripoti hii ni muhtasari unaoonyesha matokeo na mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti kuhusiana na *"Haki za Binadamu na Wavuvi Wadogo Katika Upatikanaji na Usimamizi wa Rasilimali za Bahari Tanzania"*.

## 1.1 Maelezo ya awali

Kaya nyingi katika pwani ya Bahari ya Hindi hutegemea rasilimali za uvuvi, wakiwemo wavuvi-wanawake kwa wanaume, wanaoshiriki katika shughuli zote za uvuvi katika maisha yao ya kila siku:- ikiwemo kujipatia riziki, usalama wa chakula, kuimarisha uchumi wa maeneo ya pwani, utambulisho wa kitamaduni na kijamii.

Hata hivyo, pamoja na umuhimu wao, wavuvi wadogo wanakabiliwa na changamoto ambazo zinatishia maisha yao, njia za kujipatia riziki na mazingira ya baharia yenye viumbe hai na viumbe visivyohai. Changamoto hizo ni pamoja na:- uharibifu wa mazingira, kupungua kwa samaki bahari, uchafuzi wa bahari na mabadiliko ya tabianchi. Wakati huohuo, kuongezeka kwa miradi ya uchumi wa buluu, utalii, na wavuvi wakubwa kumeongeza ushindani wa kutumia maeneo ya pwani na bahari. Hali hii inaweza kupunguza ufikiaji wa ardhi na maeneo ya jadi ya uvuvi, na kuongeza hatari ya jamii za wavuvi wadogo kupoteza maisha yao au kukosa usalama wa kipato.

Changamoto hizi zinaonesha umuhimu wa kuangalia uvuvi mdogo kwa mtazamo wa haki za binadamu. Upatikanaji wa rasilimali za bahari, ushiriki katika maamuzi, na uwezo wa kudumisha maisha endelevu, vinahusiana moja kwa moja na haki za binadamu, kama vile haki ya kufanya kazi, haki ya usalama wa chakula, haki ya kushiriki katika masuala ya umma, haki ya kuishi katika mazingira safi na salama, usawa na kutobaguliwa.

Njia ya kusimamia rasilimali za bahari kwa kuzingatia haki za binadamu (Human Rights-Based Approach - HRBA) inahakikisha kwamba, sera na mifumo ya uongozi inayohusu usimamizi wa rasilimali za bahari, inaheshimu misingi muhimu kama ushiriki wa watu wote, usawa, uwajibikaji, na upatikanaji wa haki. Kutumia njia hii kunalinda zaidi haki za wavuvi wadogo, na kukuza usimamizi shirikishi na endelevu wa rasilimali za bahari nchini Tanzania.

**Maana ya Wavuvi Wadogo**
**Ripoti hii inapotumia neno wavuvi wadogo, inamaanisha wavuvi wanawake na wanaume wanaofanya shughuli za uvuvi mdogo, katika mnyororo wa thamani wa uvuvi ikijumuisha shughuli zinazofanyika kabla, wakati na baada ya kuvua iwe ni kwenye maji ya bahari au maji ya ndani (maziwa na mito), kulingana na mwongozo wa SSF (Small-Scale Fisheries Guidelines). Na kwa mujibu wa tafsiri ya neno "jamii ya wavuvi" iliyotolewa kwenye Kanuni za Uvuvi Na. 308 za mwaka 2009.**
**Kwa hiyo, wavuvi wadogo (SSF) ni pamoja na:-**
- **Wavuvi: Watengenezaji na wamiliki wa nyavu na vyombo vya uvuvi,**
- **Wavuvi: Wanaovua samaki moja kwa moja.**
- **Wachakataji wa samaki: Wanaosafisha, kukausha, kukaanga, kugandisha au kusindika samaki.**
- **Wafanyabiashara wa samaki: Wanaouza samaki sokoni au kusafirisha kwa wateja.**
- **Wanaopanda na kuvuna mwani Pamoja na kuuchakata na kutoa mafuta na unga**

## 1.2 Malengo na Wigo wa Ripoti

Ripoti hii inalenga mambo matatu makuu:

1. Kueleza changamoto za haki za binadamu zinazowakabili wavuvi wadogo katika upatikanaji na usimamizi wa rasilimali za bahari, hasa wale walio katika mazingira hatarishi zaidi.

2. Kutambua mifumo muhimu ya sheria, sera na ya kitaasisi inayohusu upatikanaji na usimamizi wa rasilimali za bahari, na kuangalia kama zinatekeleza wajibu wa Tanzania kuhusu masuala ya haki za binadamu.

3. Kuanisha mbinu bora za utekelezaji, fursa mpya, pamoja na kuanisha suruhu za changamoto zinavyoweza kuathiri wavuvi wadogo kutokana na sera mpya au njia mpya za kusimamia rasilimali bahari na maeneo ya pwani.

Kutokana na uchache wa rasilimali, ripoti hii imejikita kwenye jamii ya wavuvi wadogo wa Tanzania Bara na mfumo wa ikolojia wa maji bahari. Maeneo yaliyohusika ni:- Msimbati na Msangamkuu (Wilaya ya Mtwara vijini, Mkoa wa Mtwara), Somanga (Wilaya ya Kilwa, Mkoa wa Lindi), Moa Wilaya ya Mkinga,  na Kigombe Wilaya ya Muheza, Mkoa wa Tanga.

# 2. MASUALA MUHIMU YA USIMAMIZI WA BAHARI KWA MTAZAMO WA HAKI ZA BINADAMU

Kanuni za haki za binadamu ni mwongozo mkuuunaotokana na sheria za kimataifa za haki za binadamu. Kanuni hizi hutumika kwa kuzingatia mtazamo wa haki za binadamu katika shughuli za maendeleo. Ripoti hiiinachambua kanuni tano (5) muhimu za kuhakikisha kuwa,usimamizi wa rasilimali za bahari unazingatia mtazamo wahaki za binadamu.[1]

## KANUNI TANO ZA HAKI ZA BINADAMU

1

### ULINGANIFU

Kuhakikisha **sheria na taratibu zinafuata masharti ya haki za binadamu** yaliyokubaliwa kimataifa.

2

### USHIRIKISHWAJI

Kuhakikisha kila mtu bila kubaguliwa, **anashirikishwa** katika maamuzi yanayohusu maisha yake

3

### KUTOKUBAGUA

Kuwepo kwa usawa na **kutokubaguliwa**

4

### UWAJIBIKAJI

Kuwepo kwa **uwajibikaji na upatikanaji wa haki**

5

### UWAZI

**Uwazi na Upatikanaji wa taarifa**

Kanuni hizi zinatafsiriwa katika vipengele muhimu vifuatavyo: -

- Kuheshimu na kukuza haki za binadamu, kuhakikisha usimamizi na sera zinazohusiana na usimamizi wa bahari zinaendana na viwango vya haki za binadamu, na kushughulikia vikwazo vya kimuundo vinavyozuia makundi yaliyotengwa kufurahia haki zao.

- Ushiriki kamilifu wa wavuvi wadogo katika maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu, upangaji wa matumizi ya bahari (Marine Spatial Planning - MSP), uhifadhi na usimamizi wa uvuvi. Ushiriki huu si haki ya jamii za wavuvi pekee, bali pia ni njia ya kuhakikisha usimamizi bora na umiliki wa pamoja wa mipango endelevu.

- Kudumisha kanuni ya usawa na kutokubagua katika usimamizi na sera zinazohusiana na usimamizi wa bahari. Hii ni muhimu ili kushughulikia athari mbalimbali za haki za binadamu ambazo wavuvi wadogo hukutana nazo. Wafanyakazi wahamiaji katika uvuvi, wanawake, vijana na watoto ni miongoni mwa makundi yanayokumbana na unyonyaji na kutengwa katika sekta ya uvuvi.

- Kuongeza uwajibikaji na upatikanaji wa haki kwa kuhakikisha kwamba wavuvi wadogo wanaweza kudai haki zao ikiwemo fidia, na nafuu nyingine za kisheria kupitia mifumo ya uwajibikaji na utoaji haki. Hii ni muhimu kwani wavuvi wadogo wanakumbana na ukiukwaji wa haki zao za umiliki wa maeneo ya uvuvi, na pia matumizi ya nguvu kupita kiasi yanayofanywa na mamlaka.

- Kuimarisha uwazi na upatikanaji wa taarifa katika usimamizi na sera zinazohusiana na bahari. Hii ni sharti la msingi kwa ushiriki kamili wa jamii za wavuvi wadogo. Taarifa kuhusu sera, mipango na hatua zinazohusiana na usimamizi wa bahari na uvuvi lazima ziwe rahisi kueleweka na zipatikane kwa wadau wote.

Uzingatiaji wamtazamo wa haki za binadamu katika usimamizi wa bahari unaweka uwiano sawa, baina ya mamlaka zinazosimamia haki (watendaji wa serikali) na wadai haki (wavuvi wadogo). Hii huwajengea uwezo wasimamizi wa haki kutekeleza haki za binadamu na wavuvi wadogo kudai haki zao.

# 3. USIMAMIZI WA HAKI MILIKI

Haki za umiliki wa maeneo ya uvuvi ni haki za binadamu. Wavuvi wadogo wana haki ya ufikiaji wa ardhi na rasilimali za asili zilizopo baharini. Haki hizi zinaathiri moja kwa moja maisha ya wavuvi wadogo kufurahia haki zao za kiuchumi, kijamii na kitamaduni, kama vile haki ya kupata chakula, haki ya kiwango bora cha maisha, na haki ya utambulisho wa kitamaduni. Utambuzi wa kisheria wa haki za umiliki wa wavuvi wadogo ni muhimu kwa mtazamo wa haki za binadamu.

Zaidi ya hayo, Mwongozo wa Hiari wa Wavuvi Wadogo (SSF-Guidelines) unaeleza kwamba, jamii za wavuvi wadogo zinahitaji kuwa na haki za umiliki wa rasilimali ambazo ndizo msingi wa: - *ustawi wa kijamii na kitamaduni; maisha yao ya kila siku; na maendeleo endelevu*[2]

Katika muktadha wa uvuvi mdogo, dhana ya haki za umiliki zinahusu haki za kutumia ardhi na maji kwa ajili ya shughuli za uvuvi[3]. Haki hizi hufungamana kwa karibu: bila ardhi ya kufikia maeneo ya uvuvi, kuweka boti, kuhifadhi nyavu na vifaa vingine, pamoja na kufanya shughuli muhimu kabla na baada ya kuvua, haki ya kufikia rasilimali za baharini hupoteza maana.

## Haki za Binadamu

Haki za umiliki wa maeneo ya uvuvi zinajumuisha pia haki zifuatazo

i. Haki ya kiwango bora cha maisha. Hii inajumuisha haki ya kupata chakula na makazi bora kwa mujibu wa ibara ya 11 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni.

ii. Haki za ardhi na rasilimali za asili ikiwemo rasilimali za bahari. Haki hii imeelezwa katika Ibara ya 14.2.g ya Mkataba wa Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW), na Ibara ya 4.2.h, 5.1, 7.3 na 17 ya Azimio la Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Wakulima na Watu Wanaofanya Kazi Vijijini (UNDROP).

## Viwango vya Haki za Binadamu vimeainishwa kama ifuatavyo

- Wakulima na wavuvi wadogo wana haki ya kupata na kutumia rasilimali za asili zilizopo katika jamii zao kwa uendelevu ili kufurahia maisha bora. Pia wana haki ya kushiriki katika usimamizi wa rasilimali hizo (UNDROP Ibara ya 5.1);

- Wakulima na watu wengine wanaofanya kazi vijijini (wakiwemo wavuvi wadogo) wana haki ya ardhi. Hii inajumuisha haki ya kupata, kutumia, na kusimamia ardhi na maji, maeneo ya pwani, maeneo ya uvuvi, malisho na misitu kwa njia endelevu. Haki hii inalenga kuhakikisha maisha bora, makazi salama, amani na heshima, pamoja na kuendeleza tamaduni zao. (UNDROP Ibara ya 17);

- Bila kujali aina ya umiliki, kila mtu anapaswa kuwa na usalama wa umiliki na ulinzi wa kisheria dhidi ya kufukuzwa kwa nguvu, kunyanyaswa au vitisho vingine. (Maoni ya Jumla Na. 4, 1991 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kijamii, Kiuchumi na Kiutamaduni);

- Serikali lazima zihakikishe kwamba wavuvi wadogo wanapata haki salama za umiliki na upatikanaji wa haki ya ardhi na rasilimali za bahari ambazo ni muhimu kwa maisha yao ya kila siku. (Maoni ya Jumla Na. 27, 2025, na Ibara ya 84 cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kijamii, Kiuchumi na Kiutamaduni);

- Serikali zinatakiwa kuchukua hatua mahsusi kwa makundi yaliyotengwa kama vile wavuvi wadogo na wanawake wanaoishi vijijini, kwa sababu mara nyingi hukumbana na ubaguzi wa kimfumo katika kupata ardhi na rasilimali za bahari. (Maoni ya Jumla Na. 27, 2025, Ibara ya 85 Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kijamii, Kiuchumi na Kiutamaduni); na

- Serikali lazima ziheshimu na, kadiri inavyowezekana, kulinda haki za jadi za jamii za wavuvi wadogo kwenye bahari, mito, maziwa na rasilimali za uvuvi, huku zikihamasisha fursa mbadala za kipato. (Maoni ya Jumla Na. 27, 2025, Ibara ya 85 Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kijamii, Kiuchumi na Kiutamaduni)

## 3.1 Kutambuliwa kwa Haki za Umiliki wa Maeneo ya Wavuvi Wadogo na Mapungufu ya Kisheria

Sheria ya Uvuvi Sura ya 279 inatambua na kulinda mbinu za jadi za uvuvi, mahitaji na maslahi ya jamii za wavuvi wadogo. Sheria hii inasisitiza kuwa mbinu hizo za uvuvi wa uwajibikaji, zinapewa kipaumbele kisheria kwa ajili ya maisha ya jamii zinazotegemea rasilimali za uvuvi.

Mfumo wa usimamizi wa uvuvi uliogatuliwa, ambapo wavuvi wadogo hushirikiana kusimamia rasilimali za uvuvi kupitia Vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali ya Uvuvi (BMUs), ni mfano bora wa utaratibu shirikishi wa 'kutoka ngazi ya chini kwenda juu' unaolenga kuhakikisha upatikanaji, matumizi na uendelevu wa rasilimali za bahari. Vilevile Mabaraza ya Uhusiano wa Vijiji na Hifadhi za Bahari (VLCs).

Licha ya utambuzi na mifumo bora ya kitaasisi, bado kuna mapungufu ya usimamizi wa sheria na ukiukwaji wa haki za umiliki katika ngazi ya mitaa na kitaifa. Kwa mfano Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009, kama zilivyo rekebishwa mwaka 2020 zinaruhusu wavuvi wadogo kuvua ndani ya umbali wa maili mbili (2) za kipimo cha kibaharia sawa na takribani km 3.7 (two (2) neautical miles) kutoka ufukweni kwa ajili ya uvuvi wa kamba (prawns), na kukataza meli za kuvua kambamiti (prawn trawlers) kufanya kazi ndani ya umbali huo. Hata hivyo, ripoti hii imebainisha mapungufu katika utekelezaji wa kanuni hii, kwa mfano, meli za kuvua kambamiti zimeonekana zikifanya kazi ndani ya hili eneo lililokatazwa kisheria. Aidha, uwezo mdogo wa Vituo vya Ulinzi na Usimamizi wa Raslimali za Uvuvi (MCS) katika ngazi zote unadhoofisha utekelezaji wa sheria na utii wa kanuni."

Ukiukwaji mwingine wa haki za umiliki hutokea pale ambapo ujenzi wa hoteli, bandari na miundombinu mingine unasababisha jamii za wavuvi wadogo kufukuzwa au kuwekewa vizuizi katika shughuli zao za baharini na ardhini . Ufafanuzi wa kisheria ulio wazi kuhusu nini kinaunda eneo la wavuvi wadogo na haki zao, katika muktadha huo utasaidia kulinda haki za umiliki wa wavuvi wadogo, hasa katika mazingira yenye ushindani mkubwa katika utekelezaji wa dhana ya Uchumi wa Buluu kuhusiana na rasilimali za bahari na pwani.

## 3.2 Mambo Muhimu ya kuzingatia kwenye Haki za Umiliki wa Wavuvi Wadogo katika Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari

Haki za umiliki wa wavuvi wadogo zinahitaji kupewa kipaumbele maalum katika jitihada za uhifadhi wa mazingira ya bahari. Hatua za uhifadhi ni muhimu kwa ulinzi wa mfumo wa ikolojia wa bahari. Kutokana na mtazamo[4] wa haki za binadamu, mazingira ambayo hayajaharibiwa (healthy ecosystems) ni sehemu ya haki ya kuwa na mazingira safi na yenye afya. Hata hivyo, mbinu za uhifadhi zinazoibuliwa kutoka ngazi za juu kwenda chini (top-down) mara nyingi hushindwa kuheshimu haki na mahitaji ya maisha ya jamii za wavuvi wadogo. Mbinu hizo husababisha kuondoshwa katika maeneo yao, kupoteza haki za jadi za umiliki, na migongano kuhusu upatikanaji na matumizi ya rasilimali. Wadau wote wanapaswa kuzingatia mtazamo wa haki za binadamu katika usimamizi wa uvuvi na uhifadhi, ndani na nje ya maeneo ya bahari yaliyohifadhiwa (Marine Protected Areas-MPAs)

Hifadhi za Bahari nchini Tanzania zimepanga maeneo maalum, mbali na maeneo yaliyokatazwa kabisa (no-take zones), ambapo wavuvi wadogo wanaruhusiwa kuvua. Hata hivyo, maeneo mengi ya karibu na pwani yamefungwa kwa madhumuni ya uhifadhi, na mbinu za uvuvi za jadi zimewekewa mipaka.

Mtazamo wa haki za binadamu katika muktadha wa kuanzishwa maeneo ya uhifadhi wa bahari, unahitaji mashauriano, ushirikishwaji wa jamii na kuzingatia haki za umiliki kwa maeneo ya uvuvi wa wavuvi wote wanaoathirika kabla ya kuweka vizuizi. Katika baadhi ya maeneo, wavuvi wadogo wameachwa bila njia mbadala za kupata riziki. Kwa mfano wavuvi wa Kisiwa cha Mafia walieleza kuwa baadhi ya maeneo yao ya uvuvi wa jadi yamechukuliwa na Hifadhi ya Bahari, jambo linalowasukuma kuvua katika maeneo mbadala ambayo tayari yanaweza kuwa na wavuvi wengine. Aidha, wavuvi walioko nje ya mipaka ya maeneo ya uhifadhi (MPAs) hususani wavuvi wadogo wanaohama, mara nyingi huondolewa katika maeneo, hata kama kihistoria walikuwa wakitumia maeneo hayo kabla hayajatangazwa rasmi kama maeneo yaliyohifadhiwa.[5]

Ni muhimu kwamba mchakato wa kuanzisha hifadhi za bahari na maeneo tengefu uzingatie mtazamo wa haki za binadamu. Hatua hii itahakikisha viwango vya haki za binadamu vinaheshimiwa kupitia ushiriki wa kutosha wa jamii, mashauriano ya wazi, na fidia pale ambapo upatikanaji wa rasilimali na uwezo wa kupata kipato unapotea. Uzingatiaji huu si muhimu tu kwa kutimiza wajibu wa haki za binadamu, bali pia ni msingi wa kuhakikisha uhifadhi unakuwa na ufanisi kwa msaada wa jamii na kuzuia wavuvi wadogo kuingia katika umaskini zaidi.

## 3.3 Mapungufu katika Fidia kwa Wavuvi Wadogo wanaopoteza Haki za Umiliki wa Bahari

Sheria ya Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu, Sura ya 146, inaruhusu serikali kutwaa ardhi, kwa madhumuni ya kuanzisha hifadhi za bahari chini ya Sheria ya Utwaaji Ardhi Sura ya 118. Ingawa fidia ya ardhi hufuata masharti ya sheria ya ardhi iliyopo, kuna pengo la kisheria kuhusu fidia kwa kupoteza haki za umiliki wa rasilimali za bahari. Sheria ya uvuvi haielezei namna ya kuwahamisha wavuvi wadogo na kuwapa fidia kwa kupunguzwa kwa maeneo ya uvuvi. Katika baadhi ya maeneo, jamii za wavuvi wadogo huondolewa kutoka kwenye ardhi za pwani na maeneo yao ya jadi ya uvuvi kwa ajili ya miradi ya utalii, hoteli, gesi au uchimbaji wa madini bila kulipwa fidia.

Serikali ina wajibu wa kulinda haki za wavuvi wadogo, ikiwemo haki ya kupata suluhisho wanapodhulumiwa, na pia kudhibiti shughuli za sekta binafsi. Biashara yenye uwajibikaji inahitaji kufuata mtazamo wa Haki za Binadamu (Human Rights Due Diligence – HRDD), ambao unahusisha kutambua na kupunguza athari, pamoja na kuweka hatua za kurekebisha madhara katika shughuli zao zinazogusa jamii na mazingira kwa ujumla.

Kadri maeneo ya bahari yaliyohifadhiwa, maendeleo ya pwani na uwekezaji unaohusiana na uchumi wa buluu unavyoongezeka, wavuvi wadogo wanakabiliwa na hatari ya kuondolewa katika maeneo yao ya asili kutokana na kuongezeka kwa ushindani juu ya matumizi ya maeneo ya bahari. Ingawa miradi hii inalenga kukuza uendelevu na ukuaji wa uchumi, inaweza kusababisha kukiukwa haki za umiliki wa wavuvi wadogo. Hali hii si masuala ya utawala pekee, bali pia ni masuala ya haki za binadamu yanayohusiana na haki za umiliki, chakula, kazi, kiwango cha maisha kinachokubalika, utamaduni, ushiriki na ulinzi dhidi ya kuondolewa bila sababu. Mifano kutoka Msumbiji , Kenya  na Ufilipino  inaonyesha kuwa mbinu shirikishi na wazi zinaweza kuimarisha uhifadhi, na kulinda haki za binadamu za jamii za wavuvi wadogo[9]

## 3.4 Mapendekezo

i. Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, iimarishe ulinzi wa kisheria wa haki za umiliki wa ardhi na bahari, ikiwemo kutenga maeneo maalum kwa wavuvi wadogo kwa kuzingatia haki za binadamu na Mwongozo wa Hiari wa Wavuvi Wadogo.

ii. Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Makamu wa Rais, irekebishe na kuweka mifumo ya kisheria Tanzania Bara, ili kujumuisha rasmi fidia ya kifedha, programu za kurejesha ustawi wa watu waliopoteza vyanzo vyao vya kipato, na maendeleo ya kijamii kwa wavuvi wadogo. Vipengele hivi vinapaswa kuwa masharti ya lazima wakati wa kuanzisha hifadhi za bahari, kuwekeza katika utalii, miradi ya uchimbaji baharini na uhifadhi, au shughuli nyingine zinazoweza kuzuia haki za umiliki wa baharini na kuathiri haki za binadamu.

iii. Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ishirikiane na Tume ya Haki za Binadamu na[6] Utawala[7] Bora pamoja[8] na mashirika yasiyo ya kiserikali kukuza uzingatiaji wa haki za binadamu, katika usimamizi na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi, ndani na nje ya maeneo ya bahari yaliyohifadhiwa. Hatua hii inajumuisha kuongeza uelewa wa umma kuhusu utekelezaji wa Mwongozo wa Hiari wa Wavuvi Wadogo, pamoja na utawala bora katika umiliki wa rasilimani za uvuvi na haki za wavuvi wadogo.

iv. Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) kitumie mchakato shirikishi zaidi katika kubuni maeneo ya bahari yaliyohifadhiwa. Hii inajumuisha mashauriano ya kina na wavuvi wadogo kwa kuzingatia viwango vya haki za binadamu, kuweka kumbukumbu za historia ya matumizi ya maeneo ya uvuvi, kushirikisha wavuvi katika majadiliano ya upangaji wa maeneo (zoning), na kuruhusu na kuthibiti matumizi ya maeneo hayo kwa misimu fulani kulingana na makubaliano ya pamoja."

# 4. HIFADHI YA JAMII KWA WAVUVI WADOGO

Upatikanaji wa hifadhi ya jamii, huduma za afya na huduma nyingine za kijamii kwa wavuvi wadogo ni muhimu kwa kuimarisha usawa, na kuongeza uwezo wao wa kustahimili changamoto wanapokabiliana na uharibifu wa mazingira, kupungua kwa samaki, uchafuzi wa bahari, pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi.

## Haki za Binadamu

Haki ya kupata hifadhi ya kijamii. Hii ni haki ya binadamu ya ulimwengu wote na pia ni haki ya kikatiba kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Ibara ya 11(1) ya Katiba inaeleza kuwa: -

*"Mamlaka ya dola itaweka masharti yanayofaa kwa ajili ya kutekeleza haki ya mtu ya kufanya kazi, kujielimisha na kupata ustawi wa kijamii wakati wa uzee, ugonjwa au ulemavu na katika hali nyingine za kushindwa kujitegemea; bila kuathiri haki hizo, mamlaka ya dola itaweka masharti ya kuhakikisha kuwa kila mtu anapata riziki yake"*

Haki ya kupata hifadhi ya kijamii pia imewekwa wazi katika nyaraka mbalimbali za kimataifa, na za kikanda za Afrika zinazohusu haki za binadamu, ikiwemo katika Ibara ya 9 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni.

Hifadhi ya Jamii' (Social Security) au 'Ulinzi wa Kijamii' (Social protection) mara nyingi hutumika kwa kubadilishana maana, zikihusu dhana moja. Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (African Charter on Human and Peoples' Rights – ACHPR) unatambua kuwa hifadhi ya kijamii imejumuishwa ndani ya dhana ya ulinzi wa kijamii, ambayo inahusu wigo mpana wa hatua zilizowekwa kulinda watu dhidi ya hatari mbalimbali".

## Viwango vya Haki za Binadamu

- Serikali zinapaswa kutambua haki za wakulima na wavuvi wadogo kupata hifadhi ya kijamii, ikiwemo bima ya kijamii. Kwa kuzingatia mazingira ya kitaifa, serikali zinapaswa kuanzisha au kudumisha mifumo ya hifadhi ya jamii yenye dhamana za msingi. Dhamana hizi zinahakikisha kwamba, kila mwenye uhitaji anapata huduma muhimu za afya na usalama wa kipato cha kawaida (UNDROP Ibara ya 22.3).
- Serikali zinapaswa kuchukua hatua mahsusi na zenye kulenga makundi fulani ili kutekeleza hatua kwa hatua haki ya hifadhi ya jamii. Kipaumbele kinapaswa kutolewa kwa wale waliopo katika mazingira hatarishi, wakiwemo wanawake, wafanyakazi walio katika ajira zisizo na uhakika, na wale walio katika sekta isiyo rasmi kama wavuvi wadogo (Maoni ya Jumla Na. 27 (2025), ya Mkataba wa Kijamii, Kiuchumi na Kiutamaduni, aya ya 56).

- Serikali lazima zihakikishe mifumo ya hifadhi ya kijamii ina fedha za kutosha, inaweza kustahimili changamoto za baadaye, na imeundwa kukidhi mahitaji ya muda mrefu kwa kutumia rasilimali zilizopo. Ikiwa rasilimali za kitaifa hazitoshi, serikali zinapaswa kutafuta msaada na ushirikiano wa kimataifa ili kuhakikisha kunakuwepo na mifumo endelevu ya hifadhi ya jamii (Maoni ya Jumla Na. 27 (2025), ya Mkataba wa Kijamii, Kiuchumi na Kiutamaduni, aya ya 57)

## 4.1 Maendelo Chanya na Mapungufu katika Hifadhi ya Jamii kwa Wavuvi Wadogo

Ripoti imebaini kuwa hakuna mifumo rasmi ya hifadhi ya jamii kwa wavuvi wadogo. Jamii nyingi za wavuvi wadogo, hususan kata ya Moa, Wilaya ya Mkinga Mkoani Tanga zinakabiliwa na changamoto za kiuchumi kutokana na upatikanaji mdogo wa samaki, magonjwa au majeraha. Ukosefu huu wa hifadhi ya jamii unadhoofisha ustahimilivu wa jamii za wavuvi wadogo na kuongeza utegemezi wao kwa rasilimali za bahari ambazo mara nyingi hupungua.

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), pamoja na benki mbalimbali wako katika mchakato wa kuanzisha mifumo maalum ya hifadhi ya jamii kwa wavuvi wadogo. Wavuvi wadogo wa Mtwara na Lindi wameonyesha utayari wa kujiunga na mifumo hiyo, na walipendekeza kufanyika kikao na NSSF, ili kujifunza zaidi kuhusu hifadhi ya kijamii na mifumo inayowafaa.

Wavuvi wadogo wanaweza kufikia hifadhi ya jamii kupitia kujiunga na mifuko rasmi, program za ustawi wa jamii, na ubunifu wa kijamii kamama VICOBA na vyama vya ushiriki.

## 4.2 Mapendekezo

i Serikali, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, ihakikishe kuwa wavuvi wadogo, pamoja na wafanyakazi wa sekta ya uvuvi na wale walio katika ajira zisizo rasmi au za msimu, wanajumuishwa katika mifumo sahihi ya hifadhi ya jamii.

ii. Wizara ya Mifugo na Uvuvi ifanye mashauriano na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), ili kubuni mifumo rahisi ya hifadhi ya jamii kwa wavuvi wadogo. Mifumo hii inapaswa kuendana na mazingira ya kazi na hatari wanazokabiliana nazo, kama vile athari za hali ya hewa, kupoteza vitendea kazi vya uvuvi au changamoto za kiafya, huku ikizingatia mahitaji ya wanawake na makundi maalum.

# 5. USIMAMIZI ENDELEVU WA UVUVI

Usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari ni muhimu katika kuhakikisha mifumo ikolojia ya bahari iliyo salama na endelevu. Wavuvi wana haki ya kunufaika na mazingira ya bahari yaliyo safi, salama na endelevu kama sehemu ya haki yao ya mazingira bora, haki ya kupata chakula, haki ya maisha yenye hadhi, pamoja na utambulisho wao wa kitamaduni. Uvuvi kupita kiasi, uvuvi haramu na uchafuzi wa mazingira vinatishia utekelezaji wa haki za binadamu.

## Haki za Binadamu

- **Haki ya mazingira safi na endelevu.** Haki hii imefafanuliwa katika Azimio la Baraza la Haki za Binadamu Namba 48/13 la mwaka 2021 na Azimio la Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa Namba 76/300 la mwaka 2022. Haki hii pia imo katika Ibara ya 24 ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu, na Ibara ya 18.1 ya Itifaki ya Maputo kuhusu Haki za Wanawake Afrika.

- **Haki ya uhifadhi na ulinzi wa mazingira, na uhifadhi na matumizi endelevu ya baioanuwai** (UNDROP Ibara ya 18 na 20).

- **Haki ya kiwango cha maisha kinachokidhi mahitaji, ikijumuisha chakula na makazi** (Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii, na Kiutamaduni-ICESCR Kifungu cha 11).

## Viwango vya Haki za Binadamu

- Wakulima na watu wengine wanaofanya kazi vijijini (wakiwemo wavuvi) wana haki ya kuhifadhi na kulinda mazingira pamoja na kusimamia rasilimali wanazotumia (ikiwemo rasilimali za bahari) (UNDROP Ibara ya 18.1).

- Serikali zinapaswa kuchukua hatua stahiki, kwa kuzingatia wajibu wake wa kimataifa, ili kuhifadhi, kuzuia upotevu na kuhakikisha matumizi endelevu ya baioanuwai kwa madhumuni ya kutekeleza haki za wakulima na watu wengine wanaofanya kazi maeneo ya vijijini wakiwemo wavuvi (UNDROP Ibara ya 20.1).

- Serikali lazima zihakikishe ushiriki wa jamii za wavuvi katika kubuni, kutekeleza na kufuatilia sheria na sera za usimamizi wa mazingira zinazohusu usimamizi wa rasilimali za bahari (Maoni ya Jumla ya CESCR Na. 27 (2025), aya ya 84).

- Kwa kutambua mchango muhimu wa wavuvi katika matumizi endelevu na usimamizi wa rasilimali za uvuvi na mifumo ikolojia. Serikali lazima zilinde na kuendeleza maarifa ya kitamaduni, ubunifu na mbinu za wavuvi (Maoni ya Jumla ya CESCR Na. 27 (2025), aya ya 84).

## 5.1 Athari za Uvunaji uliokithiri wa Rasilimali za Bahari

Taarifa za tafiti mbalimbali nchini Tanzania, zimeonyesha ongezeko la shughuli za uvuvi. Taarifa hizi ni pamoja na:- zinazotoka Serikalini, TAFIRI[10]Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa, wavuvi wadogo, mashirika ya kiraia na yasiyo ya kiserikali, tafiti hizi zinaonesha kupungua kwa uwingi wa samaki, mavuno madogo, kushuka kwa mapato, kupanda kwa bei ya samaki, na kufungwa kwa baadhi ya viwanda vya usindikaji wa samaki na mazao yake.

Ripoti hii inaonesha kuwa Tanzania imeanzisha hatua kadhaa za kisheria na kisera kukabiliana na uvuvi uliokithiri. Hatua hizo ni pamoja na kuanzishwa kwa Vikundi vya Kusimamia Raslimali ya Uvuvi (BMUs), Maeneo Shirikishi ya Usimamizi wa Raslimali ya Uvuvi (CFMAs), Hifadhi za Bahari, na Maeneo Tengefu, upangaji wa maeneo ya matumizi ya rasilimali (MSP), pamoja na doria na kusimamia utekelezaji wa sheria (MSC).

Hata hivyo, changamoto bado zipo, ikiwemo utekelezaji hafifu wa sheria, upungufu wa maafisa uvuvi, rasilimali fedha, rushwa, utoroshaji wa samaki na mazao ya uvuvi mipakani[11], ukosefu wa mifumo madhubuti ya mrejesho kwa wavuvi, na uelewa mdogo kuhusu taasisi zinazosimamia haki za binadamu kama THBUB.

## 5.2 Uvuvi Haramu

Katika maeneo ya pwani ya Tanzania, bado kuna vitendo vya uvuvi haramu kama matumizi ya nyavu zenye macho madogo, kokoro, sumu, “Juya la Kojani,” na uvuvi wa baruti. Mbinu hizi husababisha uharibifu wa mazingira ya bahari na kuathiri uendelevu wa vyanzo vya kipato kwa jamii ya wavuvi.

Ingawa Tanzania ina sheria zinazozuia matumizi ya vilipuzi, sumu, na uvuvi usio ratibiwa, utekelezaji wake bado ni mdogo. Sheria ya Uvuvi pia imeweka adhabu kali ikiwemo faini na vifungo, lakini kiwango cha utekelezaji kinatofautiana kati ya maeneo.

Aidha, katika ngazi ya kitaifa, serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilianzisha Kanda na Vituo vya Ulinzi na Usimamizi wa raslimali za uvuvi.

Katika ngazi ya mamlaka ya serikali za mitaa kwenye jamii za wavuvi kuna BMU, VLCs na CFMA zenye wajibu wa kudhibiti uvuvi haramu.

Hata hivyo, taasisi hizi mara nyingi zinapitia changamoto ya kukosa fedha, vifaa na utaalamu wa kufanya doria za mara kwa mara. Mashirika yasiyo ya kiserikali kama Mwambao Coastal Community Network, Wildlife Conservation Society (WCS), Sea Sense, na World-Wide Fund for Nature (WWF), yamechangia kuimarisha juhudi hizo kwa kuziimarisha BMU na CFMA kutekeleza majukumu yao.

## 5.3 Ukosefu wa Takwimu za Kufuatilia Uwingi wa Samaki

Kutokuwepo kwa takwimu sahihi za tathmini ya uwingi wa samaki kunadhoofisha uwezo wa kufanya maamuzi sahihi ya usimamizi wa raslimali za uvuvi. Bila taarifa sahihi, ni vigumu kupanga viwango vya uvunaji, kufuatilia mabadiliko ya rasilimali, au kuzuia kupungua kwa samaki.

Kupungua kwa samaki ni suala muhimu la kuzingatia kwa muktadha wa haki za binadamu, kwa kuwa wavuvi wana haki za umiliki na matumizi ya rasilimali za uvuvi, hivyo kupungua kwa raslimali hiyo huathiri moja kwa moja utekelezaji wa haki zao za kiuchumi, kijamii na kitamaduni. Jamii za wavuvi zina elimu ya asili kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa raslimali ya uvuvi, aina ya mavuvi, maeneo ya mavuvi na mifumo ya ikolojia ambayo inaweza kusaidia ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu. Hata hivyo, BMUs nyingi hazina uwezo wa kitaalam na kifedha wa kushiriki kikamilifu katika kazi hizo, hali inayozifanya jamii husika kubaki katika hatari ya kuendelea kupoteza rasilimali na kuongeza zaidi changamoto za kiuchumi na kijamii.

## 5.4 Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari

Uchafuzi wa mazingira ya bahari ni changamoto kubwa katika ukanda wa pwani wa Tanzania. Vyanzo vya uchafuzi vinatoka ndani na nje ya sekta ya uvuvi, ikiwemo taka za plastiki, taka za viwandani, matumizi ya viuatilifu katika kilimo, pamoja na uvuvi haramu.

Tanzania imeweka mifumo ya kisheria ya kusimamia na kudhibiti uchafuzi wa mazingira kama vile Sheria ya Usimamizi ya Mazingira Sura ya 191, Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Sura ya 146, na Sheria ya Uvuvi Sura 279. Hata hivyo, ripoti hii inaonesha haja ya kupitia upya utekelezaji wa sheria hizo ili kuhakikisha usimamizi wa kina wa mazingira ya bahari na haki ya kuwa na mazingira safi, salama na endelevu

## 5.5 Mapendekezo

i. Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa itumie mtazamo wa haki za binadamu, katika utekelezaji wa sheria za uvuvi ili kudhibiti uvuvi haramu bila kuathiri haki za watumiaji halali wa rasilimali za bahari, wakiwemo wakulima wa mwani.

ii. Serikali iimarishe uwezo wa BMU na VLCs katika ukusanyaji wa takwimu, ufuatiliaji wa uwingi wa samaki, na matumizi ya elimu asili ya jamii katika uthibitishaji wa taarifa.

iii. Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na taasisi za haki za binadamu, zifanye tathmini za athari za uchafuzi mpya wa mazingira unaotokana na gesi, uchimbaji wa madini, mabwawa na shughuli nyingine kwa jamii za wavuvi. Tathmini hizo pamoja na mambo mengine, zihusishe masuala ya haki za binadamu.

# 6. USHIRIKISHWAJI WA JAMII ZA WAVUVI WADOGO

Ushiriki thabiti wa wavuvi wadogo katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi, uchumi wa buluu, upangaji wa matumizi ya bahari na uhifadhi wa rasilimali za bahari, ni njia ya kuhakikisha usimamizi bora na umiliki wa pamoja wa juhudi za kulinda na kuendeleza rasilimali za bahari.

## Haki za Binadamu

Haki muhimu zinazohusiana na ushiriki wa wavuvi wadogo na jamii kwa ujumla ni kama zifuatazo: -

- Haki ya kushiriki katika masuala ya umma. Imeelezwa katika Ibara ya 25 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa na Ibara ya 21 ya Katiba ya Jamhura Muungano wa Tanzania
- Haki ya uhuru wa kujieleza na kupata taarifa. Imeelezwa katika Ibara ya 19 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa, Ibara ya 9 ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Haki za wanawake kushiriki katika siasa na maamuzi. Zimeelezwa katika Itifaki ya Maputo Ibara ya 9, na pia haki ya wanawake kushiriki katika usimamizi na matumizi ya rasilimali za asili (Itifaki ya Maputo Ibara ya 18.2).
- Haki ya kushiriki katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Imeelezwa katika UNDROP Ibara ya 5.1 na 17, pamoja na haki nyingine zinazohusiana na ushiriki na upatikanaji wa taarifa (UNDROP Ibara ya 2.3, 5.2, 10, 11, 15.4, na 15.5).

## Viwango vya Haki za Binadamu

- Wanawake wana haki ya kuishi katika mazingira salama na endelevu (Itifaki ya Maputo Ibara ya 18.1). Nchi wanachama zinapaswa kuchukua hatua stahiki kuhakikisha ushiriki mkubwa wa wanawake katika kupanga, kusimamia na kuhifadhi mazingira, pamoja na matumizi endelevu ya rasilimali za asili katika ngazi zote (Itifaki ya Maputo Ibara ya 18.2.a).
- Serikali lazima zihakikishe ushiriki kamilifu wa watu na makundi yaliyoathirika katika kila hatua ya maamuzi. Hii inajumuisha jamii za wavuvi wadogo wanaotegemea rasilimali za bahari. Jamii hizi zinapaswa kushauriwa ipasavyo na kuwa na uwezo wa kushawishi maamuzi ya mazingira na maendeleo yanayoathiri maisha yao. (Mkataba wa Kimataifa wa Kijamii, Kiuchumi na Kiutamaduni, Maoni ya Jumla Na. 27 (2025), aya ya 77)
- Mashauriano na ushiriki wa kweli lazima yafanyike kwa nia njema na yaendelee kabla, wakati na baada ya maamuzi. Jamii za wavuvi wadogo, zinapaswa kushirikishwa kupitia wawakilishi halali, wapatiwe taarifa za wazi na kwa lugha wanayoelewa, na wapewe nafasi ya kushawishi maamuzi. Mashauriano haya hayapaswi kuwa na shinikizo wala hofu ya kulipiziwa kisasi (Mwongozo wa Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu kuhusu utekelezaji wa haki ya kushiriki katika masuala ya umma, 2018)

## 6.1 Mifumo Imara na Mapungufu ya Utekelezaji kwa Wavuvi Wadogo

Kwa ujumla, kuna sheria na sera zinazosimamia ushiriki wa wavuvi wadogo katika maamuzi ya kisera kuhusiana na usimamizi wa rasilimali za bahari, sambamba na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu. Pia kuna miundo mizuri ya kusaidia ushiriki huo katika ngazi mbalimbali. Hata hivyo, changamoto bado zipo katika kuhakikisha ushiriki thabiti na wenye maana kwa wavuvi wadogo wakiwemo wanawake katika ngazi zote.

Kuimarisha uwazi na upatikanaji wa taarifa sahihi katika usimamizi wa rasimali za uvuvi na mifumo ya kisheria na sera zinazohusiana na bahari, ni sharti la msingi kwa ushiriki thabiti wa jamii za wavuvi wadogo. Taarifa zinazohusu sheria, sera, mipango na ushiriki lazima ziwe rahisi kueleweka na zipatikane kwa wadau wote.

Sheria, sera na kanuni kama vile Sheria ya Uvuvi, Sura ya 279, Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009, na Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu, Sura ya 146, zinatekeleza haki hii katika muktadha wa usimamizi wa rasilimali za bahari.

Mpango wa Kitaifa wa kutekeleza Mwongozo wa Hiari wa Wavuvi Wadogo (NPoA-SSF Guidelines), umejumuisha kikamilifu uzingatiaji wa haki za binadamu katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Hii inahakikisha kuwa wavuvi wadogo wakiwemo wanawake na makundi yaliyotengwa, wanashirikishwa katika maamuzi na usimamizi wa rasilimali hizo. Katika ngazi ya kitaifa, Mpango huu ni nafasi muhimu ya kuimarisha ushiriki wa wavuvi wadogo katika utungaji wa sera na mchakato wa maamuzi.

Sheria ya Uvuvi, Sura ya 279 (kifungu cha 9 na 18) inataka wadau washirikishwe katika kupanga, kuendeleza na kusimamia rasilimali za uvuvi kwa kutumia mbinu shirikishi. Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu, Sura ya 146 (kifungu cha 8(5) na 14(3)) inatambua haki ya wavuvi wadogo kuwakilishwa katika usimamizi wa maeneo ya hifadhi za bahari, kupitia Kamati za Kijamii za Kusimamia na Kulinda Rasilimali za Bahari katika Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (VLCs) na Vitengo vya Kusimamia Utekelezaji wa Sheria kwenye Ngazi ya Kijiji (VEUs). Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 2015 na Mpango Kabambe wa Sekta ya Uvuvi (2021/22–2036/37), zinatambua na kuendeleza nafasi ya wavuvi wadogo katika usimamizi wa pamoja wa rasilimali za bahari.

Licha ya sera na miundo inayosimamia ushiriki wa wavuvi wadogo, baadhi ya wadau na wavuvi waliohojiwa walieleza kuwa, bado ushiriki wa wavuvi wadogo katika ngazi ya kitaifa ni mdogo. Aidha kukosekana kwa vyama imara vya wavuvi au miundo inayofanana na vyama kumetajwa kama kikwazo kikuu, kinachosababisha uwakilishi hafifu na kukosekana kwa uratibu jumuishi miongoni mwa wavuvi wadogo.[12]

Ingawa usawa wa kijinsia ni kipaumbele katika Mpango Mkakati wa kutekeleza Mwongozo wa Hiari wa Wavuvi Wadogo (NPoA-SSF Guidelines), bado utekelezaji ni mdogo wa sera zinazozingatia jinsia katika sekta ya uvuvi. Ripoti inaonyesha ushiriki hafifu wa wanawake katika mchakato wa utungaji sera, hasa katika ngazi ya kitaifa, jambo linaloashiria mapungufu katika kushughulikia mahitaji yao kikamilifu. Kuanzishwa kwa TAWFA mwaka 2019 na Dawati la Jinsia la Uvuvi mwaka 2021 katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, pamoja na ushirikiano baina ya Wizara, FAO na mashirika yasiyo ya kiserikali, kumetoa fursa ya kuimarisha ushiriki wa wanawake wavuvi wadogo katika utungaji sera za kitaifa.[13]

Ugatuzi wa usimamizi wa uvuvi kupiti, VLCs na ushirikishwaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuanzishwa kwa BMUna CFMA, unasaidia kushirikisha wavuvi wadogo katika usimamizi wa rasilimali za bahari na utungaji sera, hasa katika ngazi ya chini. Hata hivyo, utekelezaji wa usimamizi wa pamoja unatofautiana. Wakati baadhi ya miundo hii inafanya kazi vizuri, mingine haina rasilimali za kutosha na ina uongozi dhaifu.

Nafasi ya wanawake katika maamuzi bado ni ndogo kutokana na mila na desturi za kijamii, licha ya kuwepo kwa masharti ya kuhakikisha angalau asilimia 30 ya wanawake wanashiriki katika uongozi wa BMUs na VLCs. Mpango Kabambe wa Sekta ya Uvuvi unatambua mapungufu yaliyopo katika ushirikishwaji wa wadau, hususan vijana, wanawake na jamii zilizotengwa. Mpango huu unatoa kipaumbele kwa kuandaa mikakati ya kuongeza ushiriki wao, katika usimamizi wa uvuvi na maendeleo ya sekta, ili kuhakikisha manufaa ya wavuvi wadogo yanagawanywa kwa usawa.

## 6.2 Mapendekezo

1. Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ishirikiane na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs), wadau wa uvuvi, wakiwemo Asasi za Kiraia (CSOs), ili kuimarisha uongozi na uwakilishi wa wanawake katika mchakato wa maamuzi, ndani ya BMUs na pia katika ngazi ya kitaifa.

2. Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum iwezeshe kuanzishwa kwa jukwaa la kitaifa au umoja wa wavuvi wadogo litakalotumika kama chombo cha ushauri kuhusu sera za uvuvi na mchakato wa Upangaji wa Matumizi ya Bahari. Jukwaa au shirikisho hilo linapaswa kujumuisha wanawake na makundi yaliyotengwa kama wachakataji samaki na wafanyakazi katika vyombo vya uvuvi.

3. Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Mifugo na Uvuvi iandae mwongozo wa ushirikishaji wa jamii za wavuvi wadogo, kabla ya kuanzisha mpango wowote wa maendeleo unaoweza kuathiri haki zao za binadamu, ikiwemo haki ya umiliki wa maeneo ya uvuvi. Mwongozo huo unapaswa kuendana na haki ya kupata taarifa na haki ya kushiriki katika maamuzi.

# 7. USAWA WA KIJINSIA

Haki za binadamu zinaweka haki sawa kwa wanaume na wanawake katika kufurahia haki za kisiasa, kiraia, kiuchumi, kijamii na kitamaduni.

## Haki za Binadamu

- **Haki ya usawa mbele ya sheria** (ICCPR Ibara ya 26).
- **Haki ya kutobaguliwa** (ICCPR Ibara ya 2, ICESCR Ibara ya 2) na kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake na kuendeleza uwezeshaji wao (UNDROP Ibara ya 4).
- **CEDAW: Haki maalum za muda mfupi kwa wanawake** (Ibara ya 4), **Kuondoa ubaguzi dhidi ya wanawake katika maisha ya kisiasa na kijamii** (Ibara ya 7), na **Haki za wanawake katika maeneo ya vijijini (Ibara ya 14).**
- **Haki za wanawake kushiriki katika mchakato wa kisiasa na wa maamuzi** (Itifaki ya Maputo Ibara ya 9) **na haki za wanawake kushiriki katika usimamizi na matumizi ya rasilimali asilia** (Itifaki ya Maputo Ibara ya 18.2)

## Viwango vya Haki za Binadamu

- Kufanikisha usawa kati ya wanaume na wanawake katika kufurahia haki za kiraia, siasa, kiuchumi, kijamii, na kitamaduni katika maeneo ya kisera ni muhimu kwa maendeleo endelevu (Maoni ya Jumla ya CESCR Na. 27 (2025), aya ya 42).
- Nchi Wanachama zinapaswa kuchukua hatua zote stahiki kuondoa ubaguzi dhidi ya wanawake hususani wanaoishi vijijini, ili kuhakikisha usawa wa wanaume na wanawake, kwamba wanashiriki na kunufaika na maendeleo ya vijijini. Mambo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa: -

i. Kushiriki katika uundaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika ngazi zote;
ii. Kunufaika moja kwa moja na programu za hifadhi ya jamii;
iii. Kuunda vikundi vya kusaidiana na vyama vya ushirika ili kupata fursa sawa za kiuchumi kupitia ajira au kujiajiri;
iv. Kushiriki katika shughuli zote za kijamii;
v. Kupata mikopo ya kilimo, huduma za masoko, teknolojia sahihi na usawa katika maendeleo ya ardhi na kilimo pamoja na mipango ya makazi mapya ya ardhi;
vi. Kufurahia hali bora ya maisha, hususan kuhusu makazi, usafi wa mazingira, umeme na maji, usafiri na mawasiliano (CEDAW Kifungu cha 14).

- Hatua maalum zinahitajika kwa makundi yaliyotengwa zaidi vijijini, kama vile wavuvi na wanawake, kwani mara nyingi hukumbana na ubaguzi wa kimfumo katika kupata ardhi na rasilimali za baharini (Maoni ya Jumla ya CESCR Na. 27 (2025), aya ya 85).

## 7.1 Mila, Tamaduni na Upatikanaji wa Rasilimali za Bahari katika Muktadha wa Jinsia

Mila na tamaduni zinaathiri kwa kiasi kikubwa usimamizi wa umiliki wa rasilimali, hususan katika upatikanaji wa rasilimali za bahari katika muktadha wa jinsia. Katika jamii nyingi za wavuvi, mfano Kata ya Moa, Wilaya ya Mkinga, Mkoani Tanga, shughuli za uvuvi zinafanywa kwa kiasi kikubwa na wanaume, huku wanawake wakijihusisha zaidi na shughuli za mwambao wa pwani kama kilimo cha mwani na uvuaji wa pweza. Mgawanyo huu wa majukumu unawanyima wanawake fursa ya kushiriki kikamilifu katika usimamizi wa rasilimali, jambo linaloimarisha mifumo ya maamuzi inayotawaliwa na wanaume na kuwazuia kushiriki katika nafasi za uongozi katika BMU, na shughuli za uvuvi zenye kipato kikubwa. Hali hii inakinzana na taratibu za haki za binadamu kuhusiana na usawa wa jinsia katika usimamizi wa raslimali za uvuvi, kama ilivyoainishwa katika Mwongozo wa Hiari wa Uvuvi Mdogo.

Wanawake katika sekta ya uvuvi huathirika zaidi na uwekezaji katika maeneo ya pwani hususani maeneo ya kupokelea na kuchakata samaki na mazao ya uvuvi, kama ilivyoripotiwa katika Wilaya ya Mafia[14] Mkoa wa Pwani. Ingawa mifumo ya kisheria na kisera ya kitaifa inahimiza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake, ikiwemo Mwongozo wa Kitaifa wa BMU, ushiriki wao katika maamuzi bado ni mdogo licha ya kuwepo kwa kiwango cha chini cha asilimia 30 cha wanawake katika uongozi wa BMU[15]. Vikwazo vya kitamaduni, ukosefu wa fursa za uongozi na mafunzo huendelea kuzuia ushiriki wao kikamilifu.

Sera ya Taifa ya Uvuvi ya 2015 na Mpango Kabambe wa Sekta ya Uvuvi (2021/22–2036/37) zinatambua changamoto hizi, na hivyo zimeweka kipaumbele katika masuala ya ujumuishaji wa kijinsia kwenye shughuli za uvuvi[16]. Kwa muktadha huu, kuna hatua chanya ambazo Wizara ya Mifugo na Uvuvi imefanya ikiwemo kuanzisha TAWFA mwaka 2019 kwa kushirikiana na FAO na CSOs pamoja na kuanzishwa kwa Dawati la Kijinsia la Uvuvi mwaka 2021 katika Wizara hiyo[17]. Hatua hizi zinaonyesha dhamira ya Serikali ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika uvuvi katika utungaji sera, miongozo na kushiriki katika maamuzi ya usimamizi wa raslimali za uvuvi katika ngazi ya kijamii na kitaifa.

## 7.2 Ukatili wa Kijinsia

Uvunaji wa raslimali za uvuvi kupita kiasi na changamoto zinazohusiana na maisha ya jamii za wavuvi huathiri wanaume na wanawake kwa namna tofauti. Kupungua kwa samaki kunasababisha kupotea kwa kipato na hivyo kuleta athari za kijinsia, ambapo baadhi ya wanawake wasiokuwa na vyanzo vingine vya kipato zaidi ya kukusanya rasilimali za bahari au kuuza samaki, hulazimika kujihusisha na biashara ya ngono.

Tanzania ina mifumo madhubuti ya kisheria dhidi ya unyonyaji na udhalilishaji wa kijinsia, ikiwemo Penal Code (Cap. 16), Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (2007), na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (2004). Sheria hizi hutoa ulinzi wa jumla unaowahusu pia wanawake katika jamii za wavuvi.

Ukatili wa kijinsia (GBV) ni moja ya tatizo la haki za binadamu nchini Tanzania[18]. Wanawake katika shughuli za uvuvi hukumbana, na aina mbalimbali za GBV ikiwemo unyonyaji wa kingono, na udhalilishaji katika jamii za uvuvi na katika mnyororo wa thamani wa sekta ya uvuvi. Moja ya dhana iliyojitokeza ni ile ya “samaki kwa ngono”, ambapo wanawake hulazimishwa kutoa huduma za ngono ili kupata samaki au usafiri wa boti. Shirika la ‘Fishers Union Organisation (FUO), linalofanya kazi Tanzania Bara, liliripoti kuwa wanawake katika jamii za uvuvi mara nyingi huchukuliwa kama watu wa kutumika kingono na tabia ya “samaki kwa ngono” imeenea sana, huku ubakaji ukionekana kama jambo la kawaida katika baadhi ya jamii za wavuvi[19]. Vyombo vya habari pia viliripoti matukio haya.

Mnamo Agosti 2024, wauzaji na wachakataji wa samaki wa kike katika Ziwa Tanganyika, Uvinza Kigoma, walilalamikia rushwa ya ngono inayofanywa na baadhi ya wavuvi wanaodai ngono kama sharti la kupata samaki[20]. Majadiliano ya vikundi vya wanawake na wanaume Mtwara, Lindi na Tanga pia yalibainisha visa vya “samaki kwa ngono”, ambapo baadhi ya wavuvi hukataa kuuza samaki kwa wanawake bila ngono. Hali hii pia ilithibitishwa na maafisa wa uvuvi, hususan Mtwara na Lindi, pamoja na wadau waliohudhuria warsha ya kitaifa ya wadau Julai 2025 iliyoandaliwa na THBUB.

## 7.3 Mapendekezo

1. Wizara ya Mifugo na Uvuvi na wadau wa uvuvi waendelee kuimarisha vikundi na majukwaa ya wavuvi yanayowakilisha wanawake, ikiwemo TAWFA, ili kutekeleza majukumu yao katika ngazi zote, hususan katika kuelimisha haki za binadamu na kutoa mafunzo ya uongozi.

2. Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipitie upya Mwongozo wa BMU kwa kuongeza uwakilishi wa wanawake kutoka asilimia 30 ya nafasi za kuchaguliwa hadi asilimia 50, na kuandaa mafunzo na mpango wa ulezi kwa wanawake walioko BMUs, mfano kupitia programu za kitaifa za ulezi wa uongozi kwa wanawake katika sekta ya uvuvi.

3. Wizara ya Mifugo na Uvuvi na BMU waimarishe haki za wanawake za umiliki na upatikanaji wa rasilimali za bahari, na wabuni mikakati ya kuzuia unyanyasaji wa kijinsia, udhalilishaji na ukatili dhidi ya watoto katika jamii za wavuvi.

4. Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kupitia Dawati la Kijinsia na BMU, washirikiane na THBUB kushughulikia masuala ya haki za binadamu yanayohusiana na jinsia na yanayowaathiri wanawake katika jamii za wavuvi. Ushirikiano huu unapaswa kuanzisha mfumo wa utoaji taarifa kuhusu matukio au uvunjwaji wa haki za binadamu kwa misingi ya jinsia, kufanya mafunzo ya pamoja, kufanya ufuatiliaji wa kila mwaka, tafiti, na uchambuzi wa matukio ili kutoa tathmini mahsusi na mwongozo wa kisera.

# 8. UPATIKANAJI WA NAFUU ZA KISHERIA

Wavuvi wadogo wana haki ya kupata fidia au suluhisho kupitia mifumo ya uwajibikaji na vyombo vya haki vya kimahakama na visivyo vya kimahakama, wanapokumbana na ukiukwaji wa haki za binadamu.

### Haki za Binadamu

- Haki ya kupata suluhisho (Ibara ya 2.3 ICCPR),
- Haki ya usawa mbele ya sheria (Ibara ya 26 ICCPR) na
- Haki ya kutokubaguliwa (Ibara ya 2 ICCPR, Ibara ya 2 ya ICESCR

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imeweka haki ya usawa mbele ya sheria, ikiwemo ufikiwaji wa haki na haki ya kupata suluhisho lenye ufanisi kwa watanzania wote, wakiwemo wavuvi wadogo.

### Viwango vya Haki za Binadamu

- Serikali zina wajibu wa kutoa nafuu za kisheria zinazotekelezeka kwa ukiukwaji wa haki na uhuru uliowekwa katika mikataba ya haki za binadamu, kupitia mahakama, utawala, bunge au mamlaka nyingine kwa mujibu wa mfumo wa kisheria wa nchi husika (Ibara ya 2.3 cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa).

- Serikali zinapaswa kuhakikisha upatikanaji wa haki usio na ubaguzi, kwa njia za haraka, nafuu na kwa lugha nyepesi kupitia vyombo vya mahakama na utawala vilivyo huru na vyenye uwezo. Pia zinapaswa kutoa suluhisho madhubuti na la haraka, ambalo linajumuisha haki ya kukata rufaa, kurejesha hali, fidia, malipo ya uharibifu na marekebisho (UNDROP Ibara ya 12.2).

- Iwapo haki za kiuchumi, kijamii au kitamaduni zitavunjwa kwa sababu ya uharibifu wa mazingira, serikali lazima zihakikishe kuwa, waathirika wanapata njia za haraka, nafuu na zenye ufanisi za kutafuta haki kupitia mahakama au njia nyingine zisizo za mahakama. Waathirika wanapaswa kupata suluhisho kamili, ikiwemo kurejeshewa mali au hali iliyopotea, kulipwa fidia, kupata huduma za kurekebisha madhara, na kuhakikishiwa kwamba madhara hayo hayatajirudia tena.

## 8.1 Vikwazo vya upatikanaji wa nafuu za kisheria kwa wavuvi wadogo

Tanzania ina mfumo imara wa kisheria, sera na taasisi unaolinda haki ya nafuu za kisheria pale mtu anapodhulumiwa. Katika sekta ya uvuvi, Sheria ya Uvuvi, Sura ya 279 na Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009 zinaeleza namna migogoro inavyoweza kutatuliwa.

Mfumo wa kisheria na kisera pia unaruhusu njia mbadala za kutatua migogoro ambazo zinawapa watu, wakiwemo wavuvi wadogo, nafasi ya kusuluhisha migogoro nje ya mahakama kwa kutumia mbinu kama usuluhishi wa maridhiano, upatanishi na usuluhishi wa maamuzi.

Aina za migogoro iliyoainishwa katika jamii za wavuvi wadogo ni pamoja na wavuvi dhidi ya wakulima wa mwani, dhidi ya wawekezaji wa mahoteli na wawekezaji wengine wa pwani (wanaozuia upatikanaji wa maeneo yao ya jadi ya uvuvi); uharibifu wa ikolojia na upatikanaji wa rasilimali kutokana na utafiti wa upatikanaji wa gesi na mafuta; na dhidi ya meli za wavuvi wakubwa wa kambamiti[21]. Aidha hatua za kutenga maeneo ya hifadhi ya bahari (MPAs) pia zinaweza kuongeza migogoro endapo mashauriano na fidia hazitakuwa za kutosha.

Kuna vikwazo vingi vinavyowazuia watu kupata haki kupitia mfumo rasmi wa mahakama. Baadhi ya vikwazo hivyo ni rushwa, uhaba wa watendaji wa haki, gharama kubwa za uwakilishi wa kisheria, kesi kuchukua muda mrefu, upatikanaji mdogo wa msaada wa kisheria, uelewa mdogo kuhusu sheria na taratibu, pamoja na ucheleweshaji wa utoaji wa haki. Vikwazo hivi vinawafanya wavuvi wadogo washindwe kupata njia rahisi, nafuu na madhubuti za kutatua migogoro ya haki za umiliki na migogoro mingine. Mara nyingi, migogoro ya wavuvi wadogo haimalizwi mahakamani kwa sababu ya vikwazo hivi.

Mbinu za kutatua migogoro katika ngazi ya jamii zina nafasi muhimu katika kutatua migongano dhidi ya rasilimali. Migogoro inaweza kupelekwa kwenye BMU na CFMA. Pia mamlaka za serikali za mitaa kama kijiji, kata na wilaya zina mamlaka ya kutatua migogoro bila haja ya kwenda mahakamani. Sheria ya Hifadhi za Baharii na Maeneo Tengefu, Sura ya 146 inaruhusu kukata rufaa kwa Waziri anayehusika na hifadhi za bahari na maeneo tengefu endapo kutakuwa na ukiukwaji wa haki.

Ripoti imebaini kuwa wavuvi wadogo wengi wanaona njia mbadala za kutatua migogoro zina ufanisi zaidi kuliko njia za mahakama. Hata hivyo, wasiwasi uliibuliwa kuhusu mbinu hizi kutokuwa rasmi, kwani mara nyingi hazina taratibu zilizoandikwa na hazina mamlaka ya kisheria ya kutoa fidia na uwezo mdogo wa kutekeleza maamuzi yanayotolewa na BMU. Aidha, ripoti ilibaini kuwa baadhi ya wavuvi wadogo waliohojiwa walieleza kuwa hawaitumii Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) kama njia mbadala ya kutatua migororo kwasababu hawaifahamu.

## 8.2 Mapendekezo

i. Serikali, kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mamlaka za Serikali za Mitaa, na wadau wa uvuvi ifanye mafunzo ya kujenga uwezo kwa wavuvi wadogo kuhusu mbinu za kutatua migogoro, ikiwemo za kimahakama na zisizo za kimahakama ikiwemo THBUB.

ii. Wizara ya Mifugo na Uvuvi ijenge uwezo na kuhamasisha BMU kutoa taarifa ya matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu kwenye Ofisi za THBUB, makao makuu Dodoma, ofisi ya Zanzibar, na ofisi za matawi zilizoko Mtwara, Pemba, Mwanza, Tabora na Dar es Salaam. Utoaji wa taarifa unapaswa kufanyika kila robo mwaka kwa kutumia fomu maalum, itakayojumuisha maelezo kuhusu aina ya tukio, makundi yaliyoathirika, na hatua zilizochukuliwa kufuatilia tukio hilo.

iii. Serikali, kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu), isimamie utekelezaji wa sheria na viwango vya kazi vinavyohusiana na mikataba ya ajira ili kuongeza uwezo wa wavuvi wadogo kudai haki kupitia njia za kisheria na kiutawala.

iv. Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Makamu wa Rais, pamoja na wizara, idara na taasisi nyingine, kuhakikisha taratibu sahihi zinafuatwa na fidia ya haki inatolewa wakati wa kutekeleza shughuli zinazoweza kuzuia haki za umiliki, kusababisha watu kuhamishwa, au kuathiri haki za binadamu za jamii za wavuvi wadogo.

# 9. UCHUMI WA BULUU NA MATUMIZI YA BAHARI

Ni muhimu kuhakikisha jamii za wavuvi na vizazi vijavyo wananufaika na faida zitokanazo na rasilimali za Uchumi wa Buluu kwa kulinganisha mifumo ya Sera ya Uchumi wa Bluu, Mpango wa Matumizi ya Bahari, na kutumia miongozo ya haki za binadamu, Hili linaweza kufanikishwa kwa kutumia mbinu ya mtazamo wa haki za binadamu, katika uandaaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya maeneo ya bahari.

## Haki za Binadamu

- **Haki ya kiwango cha maisha bora, ikijumuisha haki ya chakula na makazi** (ICESCR Ibara ya 11).

- **Haki ya ardhi na rasilimali asilia** (ikiwemo rasilimali za bahari) (CEDAW Ibara ya 14.2.g, na UNDROP Ibara ya 4.2.h, 5.1, 7.3 na 17).

- **Haki ya mazingira safi, yenye afya na endelevu** (Azimio la Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za BInadamu (HRC) 48/13 la mwaka 2021 na Azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA) 76/300 la mwaka 2022, ACHPR Ibara ya 24 na Itifaki ya Maputo Ibara ya 18.1).

- **Haki za uhifadhi na ulinzi wa mazingira, na uhifadhi na matumizi endelevu ya baioanuwai** (UNDROP Ibara ya 18 na 20).

- **Haki ya kushiriki katika mijadala mbalimbali ya hadhara** (ICCPR Ibara ya 25, Katiba ya Tanzania, Ibara ya 21).

- **Haki ya uhuru wa kujieleza na kupata taarifa** (ICCPR Ibara ya 19, ACHPR Ibara ya 9, Katiba ya Tanzania, Ibara ya 18).

- **Haki za wanawake kushiriki katika siasa na mchakato wa maamuzi** (Itifaki ya Maputo Ibara ya 9) na **haki za wanawake kushiriki katika usimamizi na matumizi ya rasilimali asilia** (Itifaki ya Maputo Ibara ya 18.2).

## Viwango vya Haki za Binadamu

- Maoni ya Jumla ya CESCR Na. 27 (2025) yanasisitiza kwamba usimamizi wa mazingira na mipango ya maendeleo lazima uheshimu, ulinde na kutekeleza haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni, hususan kwa jamii zinazotegemea rasilimali asilia kwa maisha yao, kama jamii za wavuvi.

- Serikali lazima zihakikishe kwamba matumizi mabaya ya rasilimali asilia, iwe na taasisi za kitaifa au za kigeni, yasimamiwe ipasavyo ili kuwepo na usawa na haki, kwa kuimarisha haki za binadamu (CESCR Maoni ya Jumla Na. 27 (2025), aya ya 46).

- Serikali zina wajibu wa kuhakikisha ulinzi wa kisheria katika maamuzi yote yanayohusiana na matumizi mabaya ya rasilimali asilia, ikiwemo kuhakikisha ushiriki, upatikanaji wa taarifa kwa wakati na kwa lugha rahisi ya kueleweka, na kuzingatia misingi ya haki za binadamu katika mchakato wa utoaji leseni na mikataba (CESCR Maoni ya Jumla Na. 27 (2025), aya ya 47).

- Utoaji wa leseni au vibali lazima utanguliwe na tathmini huru na shirikishi ya athari za mazingira na haki za binadamu, yenye lengo la kubaini madhara yanayoweza kutokea kwa mujibu wa sheria za kimataifa za haki za binadamu na mifumo ya ndani. Tathmini hizi zinapaswa kuongoza maamuzi na ziambatane na mifumo madhubuti ya kupata suluhu, hususan kwa jamii zilizoathirika (CESCR Maoni ya Jumla Na. 27 (2025), aya ya 47).

## 9.1 Mtazamo wa Haki za Binadamu katika Uchumi wa Buluu na Mpango wa Matumizi ya Bahari

Ripoti inatoa angalizo kwamba utekelezaji wa Uchumi wa Buluu na Mpango wa Matumizi ya Bahari (MSP), unaweza kuongeza hali ya kutengwa kwa wavuvi wadogo na pia kuongeza ushindani juu ya matumizi ya maeneo ya bahari.

Tanzania ilipitisha Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu Mwaka 2024, ambayo imeweka wazi kuwa MSP ni nyenzo muhimu ya kuweka urari wa vipaumbele vinavyokinzana kama uhifadhi, shughuli za kujikimu na maendeleo ya kiuchumi. Mchakato wa kuandaa MSP umeanza kwa kuandaa Mwongozo wa Uandaaji wa Mwaka 2023. Mwongozo huu unaoongozwa na Ofisi ya Makamu wa Rais na unasisitiza umuhimu wa ushiriki wa jamii, hususan wavuvi, katika mchakato mzima.

Mchakato wa MSP unatoa fursa kwa wavuvi, kama vile kutambuliwa kwa haki, kuboresha maisha na maendeleo ya kiuchumi, lakini pia unahusisha athari, ikiwemo ukiukwaji wa haki za umiliki, haki ya kushiriki katika maamuzi na haki ya mazingira safi, na endelevu. Matukio ya wavuvi kuondolewa kwenye maeneo yao ya asili na uwekezaji katika sekta shindani kama utalii, madini, uvuvi wa viwanda (coastal squeeze), ni hatari inayoweza kujitokeza Tanzania kama ilivyo kwingine, endapo haki za wavuvi zitakiukwa..

Tanzania ina mifumo madhubuti ya kisera na taratibu za usimamizi shirikishi kupitia BMU. Ni muhimu kuimarisha misingi hii katika mchakato wa usimamizi wa MSP na kuhakikisha BMU zinahusishwa kikamilifu, kujengewa uelewa na uwezo wa kutetea haki za umiliki za wavuvi, ikiwemo haki za binadamu za kupata taarifa na kushiriki katika maamuzi ya MSP. Hii inajumuisha kutenga maeneo ya bahari kwa mashauriano na wavuvi na kutenga maeneo ya matumizi mseto yanayojumuisha uvuvi mdogo sambamba na shughuli za viwanda.

Kuongezeka kwa uvuvi mkubwa, kilimo cha mwani, uchimbaji wa madini na uzalishaji wa nishati kunaweza kuongeza ushindani wa rasilimali na migogoro inayohusisha wavuvi. Pia wavuvi wako katika hatari ya kuhamishwa kutokana na upanuzi wa MPA, utalii, uvuvi mkubwa na miradi mingine ya maendeleo. Katika muktadha huu, ni muhimu wavuvi wadogo washirikishwe ipasavyo na kushauriwa, na mifumo ya fidia isimamiwe kwa ufanisi. Vilevile, ni lazima kuhakikisha wavuvi wadogo wanapata suluhu iwapo haki zao zitavunjwa.

Bila kuwepo kwa haki za kisheria za umiliki kwa wavuvi wadogo, upatikanaji wa maeneo maalum ya uvuvi unakuwa dhaifu. Hali hii, ikichangiwa na uelewa mdogo kuhusu haki za binadamu na ukosefu wa jukwaa la kitaifa au umoja unaowakilisha wavuvi wote. Matokeo yake ni kwamba haki za umiliki za wavuvi wadogo zinadhoofika, na sauti zao hazisikiki ipasavyo katika maamuzi muhimu yanayohusu mgao na upatikanaji wa rasilimali za baharini ndani ya mchakato wa MSP.

## 9.2 Mapendekezo

i. Serikali, kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, itumie mbinu za mtazamo wa haki za binadamu (HRBA) katika michakato ya MSP, ili kulinda haki za umiliki za wavuvi wadogo, ushiriki, na kuhakikisha nafasi rasmi kwa wanawake na wavuvi wadogo.

ii. Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Mifugo na Uvuvi iandae programu mbadala za kipato zinazohusiana na uhifadhi wa bahari. Mchakato wa MSP na juhudi za uvuvi unapaswa kuzingatia athari za mabadiliko ya tabianchi, kulinda haki za binadamu, na kuhakikisha uendelevu wa kiikolojia. Hatua hizi pia zinapaswa kuendana na tamaduni za jamii husika na zisivunje haki za umiliki wa wavuvi wadogo.

iii. Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Mifugo na Uvuvi wadau wasio wa kiserikali ifanye tathmini ya kina ya athari za haki za binadamu katika sekta ya Uchumi wa Buluu ili kubaini athari kwa wavuvi wadogo na hatua za kupunguza madhara.

iv. Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Mifugo na Uvuvi itekeleze hatua za kimkakati zilizomo katika Mpango wa Taifa wa Haki za Binadamu na Biashara kuhusu "Haki za Ardhi na Rasilimali Asilia", ikiwemo uanzishwaji wa MSP.

# 10. MABADILIKO YA TABIANCHI NA ATHARI ZA MAJANGA KWA WAVUVI WADOGO

Wavuvi wadogo wana haki ya mazingira safi na salama, haki ya kupata chakula, kipato cha maisha na kiwango cha maisha kinachokidhi mahitaji. Haki hizi zote zinaweza kuathiriwa na athari za mabadiliko ya tabianchi katika mfumo wa ikolojia ya bahari.

## Haki za Binadamu

- Haki ya kuishi (ICCPR Ibara ya 6).

- Haki ya kiwango cha maisha kinachokidhi mahitaji, ikiwemo chakula na makazi (ICESCR Ibara ya 11).

- Haki ya afya bora (ICESCR Ibara ya 12).

- Haki ya kushiriki katika kubuni na kutekeleza sera za kitaifa na za kijamii za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza athari zake (UNDROP Ibara ya 18.3).

## Viwango vya Haki za Binadamu

- Jamii za wavuvi zina haki ya kushiriki katika kubuni na kutekeleza sera za kitaifa na za kijamii za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, na kupunguza athari zake, ikiwemo kutumia mbinu na maarifa asilia ya ikolojia (UNDROP Kifungu cha 18.3).

- Maoni ya Jumla ya CESCR Na. 27 (2025) yanasisitiza kwamba Serikalii lazima zilinde jamii zinazotegemea rasilimali asilia, dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa mazingira na kupotea kwa baioanuwai.

- Serikalii zina wajibu wa kushughulikia ubaguzi wa kimfumo na wa kimuundo na kulinda watu na jamii dhidi ya uvunjwaji wa haki za binadamu unaotokana na madhara ya mazingira na hatua zinazochukuliwa kukabiliana na madhara hayo. Serikali lazima zitambue na kuzingatia mahitaji ya watu na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi au yaliyotengwa, kwa kuzingatia dhana ya mwingiliano wa utambulisho wa kijamii (intersectionality), CESCR Maoni ya Jumla Na. 27 (2025), aya ya 39.

## 10.1 Mabadiliko ya Tabianchi na Athari za Haki za Binadamu kwenye Maisha ya Wavuvi wadogo

Wavuvi wadogo nchini Tanzania wako hatarini kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili, ambayo ni: - dhoruba, upepo mkali, mafuriko na kuongezeka kwa joto la bahari. Kuongezeka kwa nguvu za dhoruba kunafanya uvuvi kuwa hatari zaidi, huku mabadiliko ya joto na mikondo ya maji yakibadilisha maeneo ya mazalia na kuhama kwa samaki, jambo linalopunguza mavuvi na kuathiri sekta nzima[22]. Aidha, kuongezeka kwa joto la bahari na asidi ya bahari vinapunguza mavuno ya mwani, jambo lililothibitishwa na jamii za wavuvi[23]. Hali hii inaleta athari kubwa kwa haki za binadamu, ikiwemo haki ya chakula, kipato na maisha bora.

Tanzania imechukua hatua kadhaa za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na usimamizi wa majanga, ikiwemo kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (NCCRS) na mipango ya kitaifa ya kukabiliana na athari zake. Taasisi kama VPO (Mazingira), na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) zina jukumu la kuratibu juhudi hizi. Hata hivyo, sera nyingi hazina hatua mahsusi zinazolenga mahitaji ya wavuvi wadogo. Mpango Kabambe wa Sekta ya Uvuvi (2021/22–2036/37) hautoi mikakati thabiti ya kujenga ustahimilivu dhidi ya majanga na tabianchi[24]. Vilevile, Sheria ya Usimamizi wa Majanga, Sura ya 242 haijajikita moja kwa moja katika sekta ya uvuvi mdogo.

Jamii za wavuvi wadogo zina uelewa mdogo kuhusu mipango ya kukabiliana na majanga, mabadiliko ya tabianchi na tahadhari za mapema kutoka TMA, mfano taarifa za upepo mkali nk. Hii inaonyesha mapungufu katika mawasiliano kati ya mamlaka na jamii za wavuvi wadogo. Upatikanaji mdogo wa taarifa za mabadiliko ya tabianchi, mifumo ya tahadhari na rasilimali za kifedha vinapunguza uwezo wa wavuvi wadogo kukabiliana na athari za majanga ya mabadiliko ya tabia nchi.

Kwa muktadha huu, wavuvi wana haki ya kulindwa dhidi ya athari za haki za binadamu zinazotokana, na athari za mabadiliko ya tabianchi na hatua zinazochukuliwa kukabiliana na athari hizo. Ni muhimu sera za kitaifa zijumuishe mahitaji mahsusi ya wavuvi wadogo, ziwape taarifa sahihi na fursa za kushiriki katika maamuzi, na kuhakikisha mifumo ya fidia na msaada wa kifedha inapatikana ili kujenga ustahimilivu wao.

## 10.2 Mapendekezo

i. Wizara ya Mifugo na Uvuvi ishughulikie mapungufu yaliyopo katika Mipango ya VPO ya kukabiliana na majanga na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa wavuvi wadogo. Mipango hiyo ijumuishe hatua mahsusi zinazolenga jamii za wavuvi kwa kuzingatia haki za binadamu na mwongozo wa NPoA-SSF Guidelines.

ii. TMA iimarishe ushirikiano wao wa moja kwa moja na BMU ili kutekeleza mifumo ya tahadhari za mapema katika ngazi za kijamii.

iii. Wizara ya Mifugo na Uvuvi ihakikishe kwamba miradi yoyote ya mikopo ya kaboni ya buluu au kijani inajumuisha ulinzi wa haki za binadamu, ushiriki madhubuti, mgawanyo kwa kuzingatia usawa, na kanuni nyingine muhimu ili kuhakikisha utekelezaji wa haki za wavuvi wadogo na kuepusha madhara kwa haki zao kutokana na miradi ya mabadiliko ya tabianchi.

# 11. URATIBU NA UJUMUISHAJI WA SERA KWA WAVUVI WADOGO

Usimamizi bora wa bahari na matumizi endelevu ya rasilimali za bahari unahitaji uratibu wa taasisi mbalimbali za serikali pamoja na ushirikiano na asasi za kiraia, jamii za wavuvi wadogo, na taasisi huru za uangalizi. Sera za sekta mbalimbali kama usimamizi wa uvuvi, ulinzi wa mazingira, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, na mipango ya Uchumi wa Buluu zinaweza kusaidia ulinzi, utetezi na uhifadhi wa haki za binadamu katika jamii za wavuvi wadogo.

### Haki za Binadamu

Uratibu na ujumuishaji wa sera kwa wavuvi wadogo inahusisha upatikanaji wa haki mbalimbali za wavuvi wadogo. Haki hizi ni: -

- Serikali lazima zipitishe sera zilizo thabiti na zenye uratibu ili kuhakikisha kuwa usimamizi wa mazingira na mipango ya maendeleo unaheshimu na kulinda haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni, hususan kwa jamii zinazotegemea rasilimali za asili. (Maoni ya Jumla Na. 27 (2025) ya ICESCR)

- Serikali zinapaswa kujumuisha mbinu zinazozingatia usawa wa kijinsia na kushirikisha serikali nzima katika sera zote za maendeleo endelevu, hususan zile zinazohusiana na kupunguza athari za majanga, mabadiliko ya tabianchi, uchafuzi wa mazingira, ulinzi wa bayoanuwai na usimamizi wa rasilimali za asili (Maoni ya Jumla Na. 27 (2025), aya ya 45 ya Mkataba wa Kijamii, Kiuchumi na Kiutamaduni).

## 11.1 Kuongeza Wigo wa Ulinzi wa Haki za Binadamu kwa Wavuvi Wadogo zaidi ya Usimamizi wa Uvuvi.

Kuna sera na mifumo mizuri mingi ya usimamizi wa uvuvi lakini utekelezaji wake haujaunganishwa vizuri. Haki za binadamu za wavuvi wadogo mara nyingi hazijumuishwi katika kupanga, kutekeleza na kufuatilia sera hizi.

Kadri sekta ya Uchumi wa Buluu inavyoendelea kukua, kutakuwa na haja ya kushughulikia changamoto za uratibu baina ya Wizara za serikali ili kuhakikisha haki za wavuvi wadogo zinajumuishwa katika sera, mipango na mikakati husika, na utekelezaji wake unafanyika kwa uratibu na kwa njia thabiti. NPoA-SSF- Guidelines unasisitiza ulinganifu wa sera, uratibu wa taasisi na ushirikiano. Moja ya hatua za utekelezaji wake ni kufanyia mapitio na kuoanisha kanuni zinazohusu uwekezaji, uvuvi na utalii.

Miundo ya taasisi inayohusisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Makamu wa Rais, na mashirika mengine ya serikali inatoa msingi wa uratibu katika usimamizi wa rasilimali za bahari na uvuvi endelevu. Aidha THBUB ina mfumo muhimu wa uangalizi kwa ajili ya kukuza na kulinda haki za binadamu nchini, ikiwemo haki zinazohusiana na ardhi na rasilimali za asili, pamoja na rasilimali za bahari.

Mpango wa NPoA-SSF Guidelines, kama ule wa wavuvi wadogo, umeweka wazi kuwa unatumia mtazamo wa haki za binadamu katika usimamizi wa uvuvi. Pia umeangazia usawa wa kijinsia, na kuunganisha sera na mifumo ya kisheria kutoka sekta nyingine. Mpango huu unataja umuhimu wa uratibu wa sera, ushirikiano wa taasisi na mashirikiano. Aidha, NPoA-SSF- Guidelines unahusisha hatua zinazolinda haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni za wavuvi wadogo, na kuunganisha sera na mifumo ya kisheria kutoka sekta nyingine kama vile Sera ya Taifa ya Wanawake na Maendeleo ya Kijinsia (2000), Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (2004), Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, na Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Umaskini (MKUKUTA II). Hii inaonyesha jitihada za kuoanisha malengo ya sekta ya uvuvi na vipaumbele vikubwa vya maendeleo ya taifa na sekta nyingine, jambo linaloashiria uratibu wa sera. Hata hivyo, masuala na wajibu wa haki za binadamu hayajumuishwi kwa uthabiti katika sera za sekta na katika utekelezaji wake, ikiwemo usimamizi wa uvuvi na upangaji wa matumizi ya bahari. Uelewa mdogo na ukosefu wa uwezo katika taasisi za sekta unaweza kuzuia utekelezaji bora wa mtazamo wa haki za binadamu katika usimamizi wa uvuvi.

## 11.2 Mapendekezo

i. Serikali, kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ichukue hatua za kuhakikisha haki za binadamu za jamii za wavuvi wadogo zinatekelezwa, na kuongeza uratibu na ushirikiano na THBUB.

ii. Serikali izijengee uwezo taasisi zinazohusika na uvuvi na uhifadhi, ikiwemo WMU, MPRU, TARIFI, VPO na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA), kwa kutoa mafunzo maalum kuhusu haki za binadamu na mtazamo wa haki za binadamu katika uvuvi na uhifadhi. Hii inapaswa kujumuisha warsha za kila mwaka, kuingiza vipengele vya mtazamo wa haki za binadamu katika mitaala ya mafunzo ya taasisi, na kutengeneza zana za ufuatiliaji ili kupima utekelezaji wake.

# REFERENCES


[1] For an introduction to the five HRBA principles, see for example, DIHR 2024. The HRBA Check - a human rights-based approach accountability mechanism. https://www.humanrights.dk/publications/hrba-check-human-rights-based-approach-accountability mechanism, and DIHR's e-course about Human Rights Based Approach (HRBA). https://training.humanrights.dk/course/view.php?id=102.

[2]Voluntary Guidelines for Securing Sustainable Small-Scale Fisheries in the Context of Food Security and Poverty Eradication (SSF Guidelines, para. 5.1)

[3] FAO. 2020. Legislating for Sustainable Small-Scale Fisheries – A guide and considerations for implementing aspects of the SSF Guidelines, Rome, and in line with recommendations and comments from UN human rights treaty bodies and special procedures.

[4] Mwaipopo, R., 2018. Review of Policies, Laws, Institutional and Regulatory Framework Governing the Fisheries Sector in Relation to SSF Guidelines

[5] Shayo et al., 2022. Local area management strategy for small pelagic (dagaa) fishery in RUMAKI seascape fishing communities through the framework of COLLABORATIVE FISHERIES MANAGEMENT AREAS (CFMAs. WWF Tanzania Country Office, Dar Es Salaam, Tanzania.

[6] https://www.mozambiquelng.co.mz/first-fisher-compensation-agreements-signed/

[7] https://www.seacology.org/project/62-kenya/

[8] https://www.cbd.int/financial/fiscalenviron/philippines-fiscalfee.pdf

[9] https://www.mozambiquelng.co.mz/first-fisher-compensation-agreements-signed/

[10] Kapapa et al.,2022. The vulnerability of fisheries-based livelihoods to climate variability and change in coastal small pelagic fishing communities in Tanzania. Marine Policy 169, 106344

[11] Ibengwe et al., 2022. Regional trade integration and its relation to income and inequalities among Tanzanian marine dagaa fishers, processors and traders. Marine Policy 137, 104975.

[12] Interview with the representative from the SSF Guidelines National Task Team.

[13] Interview with the representative from MLF.

[14] Shayo et al., 2022. Local area management strategy for small pelagic (dagaa) fishery in RUMAKI seascape fishing communities through the framework of collaborative fisheries management areas (CFMAs). WWF Tanzania Country Office, Dar Es Salaam, Tanzania

[15] Katikiro et al., 2024. The establishment, persistence, and scaling of marine community-based natural resource management in four coastal districts in Tanzania. Marine Policy 169, 106341

[16] National Fisheries Policy (supra); Fisheries Sector Master Plan (*supra*).

[17] Interview with the representative from Ministry of Livestock and Fisheries.

[18] LHRC, 2023, Tanzania Human Rights Report 2023. Available at https://humanrights.or.tz/en/news-events/Lhrc_report_2023

[19] See FUO Concept Note for Reduction of Gender-Based Violence & HIV/AIDS Infections Among the Fisher Folks Community in Islands of Sengerema District. Available at https://www.policyforum-tz.org/sites/default/files/ConceptGBVINFISHINGCOMMUNITIES.pdf.

[20] Kadislaus Ezekiel 'Rushwa ya ngono inavyowatesa wanawake ziwa Tanganyika' Radio Tadio, 30 August 2024. Available at https://radiotadio.co.tz/joyfm/2024/08/30/3240/

[21] Interview with a representative from the SSF Guidelines National Task Team; Mwakosya and Mwaka, 2021; Shayo et al., 2022

[22] Trisos et al., 2022: Africa. In: Climate Change 2022: Impacts, Adaptation and Vulnerability. Contribution of Working Group II to the Sixth Assessment Report of the Intergovernmental Panel on Climate Change

[23] Msuya et al. 2022. Coping with Climate Change to Safeguard the Seaweed Industry in Eastern Africa: Spotlight on Tanzania

[24] Mwaipopo, R., 2018. Review of Policies, Laws, Institutional and Regulatory Framework Governing the Fisheries Sector in Relation to SSF Guidelines

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

Jengo la PSSF, Mtaa wa Makole

S.L.P 1049

info@chragg.go.tz

+255 (0) 738 279 744

**Dodoma, Tanzania**

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**

Jengo la Justice Lugakingira, Kitalu Na 44, Kiwanja Na 508/509

S.L.P 75254

lhrc@humanrights.or.tz

+255 (0) 2773038/48

**Dar es salaam, Tanzania**